WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI




JARIDA MAALUM

# UZINDUZI WA MPANGO WA KITAIFA WA URASIMISHAJI MAKAZI

## YALIYOMO


**01** Mpango wa kukopesha wananchi

**02** Ardhi kuwa mtaji

**03** ARU kudhibiti makazi holela

**04** Madaftari ya migogoro ya ardhi

**05** Matukio katika picha



BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Mwenyekiti

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAANDISHI**
Munir Shemweta, Eliafile Solla, Hassan Mabuye, Magreth Lyimo



Mji wa Serikali Mtumba, S. L. P. 2908 | 40477- DODOMA | Simu: +255 262 963309/13/14 | Nukushi: +255 262 963316
Barua pepe: ps@lands.go.tz | Tovuti: www.lands.go.tz




*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi (kushoto) akipongezana na Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB Bwana Benedicto Baragomwa (kulia) wakati wa uzinduzi wa Mpango wa kitaifa wa kurasimisha makazi kwa kukopesha wananchi gharama ya kupanga, kupima na kupewa hati kwa kushirikiana na Benki ya NMB katika kata ya Igawa wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya.*

# SERIKALI YAZINDUA MPANGO WA KUKOPESHA WANANCHI KATIKA URASIMISHAJI

**Na. Hassan Mabuye,** MBEYA

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi amezindua mpango maalumu wa kuwakopesha wananchi fedha za kufanya urasimishaji wa maeneo yao kwa kipindi cha miaka miwili.

Waziri Lukuvi ameyasema hayo katika kata ya Igawa wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya wakati akizindua Mpango wa maalumu wa kukopesha wananchi gharama ya kupanga, kupima na kupewa hati kwa kushirikiana na Benki ya NMB.

Lukuvi amesema mpango huu ni wa nchi nzima ambao umeanzia hapa Mbarali kwa kuwamilikisha wananchi zaidi ya 52,000 kwa kuwa mazoezi mengi ya urasimishaji yameshindwa kufanikiwa kwa sababu baadhi ya wananchi wameshindwa kupata fedha kwa mkupuo kugharimia shilingi 150,000 za upimaji na umilikishaji.

"Nimeamua kuanzisha mpango huu kwa kushirikiana na NMB ambao watawakopesha fedha za kupanga, kupima na kuandaa hati ambazo Benki italipa 100% kwa mkupuo kisha nyinyi mtalipa taratibu na kwa awamu kwa muda wa miezi 24 yaani miaka miwili" Amesema Waziri Lukuvi.

"Baadhi ya wananchi wamekwamisha kazi hii ya urasimishaji katika maeneo mengi kwa kuwa wachache ndio wameweza kupata fedha za kugharimia upangaji, upimaji na umilikishaji kwa wakati. Sasa NMB leo hapa Mbarali wamekuja kuwakopesha wananchi gharama zote. Na ninataka zoezi kama hili lifanyike nchi nzima na wengine waige kwa kuafuata utaratibu huu" Ameongeza Waziri Lukuvi.



*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi akizungumza na wakazi wa kata ya Igawa wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya wakati wa uzinduzi wa Mpango wa kitaifa wa kurasimisha makazi kwa kukopesha wananchi gharama ya kupanga, kupima na kupewa hati kwa kushirikiana na Benki ya NMB.*

Amesema pia 90% ya wananchi wa Mbarali walikuwa hawakopesheki kwa sababu ya ardhi yao ilikuwa haijapangwa wala kupimwa. Lakini kwa mpango huu pia watakuwa na haki ya kukopeshwa na benki yoyote hapa nchini kwa kuwa watakuwa na dhamana inayotambulika kisheria ambayo ni hatimiliki ya ardhi.

Naye Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB Bwana Benedicto Baragomwa amewataka wananchi kuchangamkia fursa hii kufanya urasimishaji kupitia Benki ya NMB ambayo itafanya zoezi hili kwa kutumia matawi yake yote 226 nchi nzima kujipatia mkopo huu na kujiwezesha kiuchumi.

Kwa upande Mwingine Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maeneleo ya Makazi Bibi Mary Makondo amewahakikishia wananchi kwamba Wizara yake itasimamia kikamilifu mpango huu ambao wananchi watapewa hatimiliki za ardhi za miaka 99 na watamilikishwa kisheria.



*Baadhi ya wakazi wa kata ya Igawa wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya wakimsikiliza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi wakati akizungumza katika uzinduzi wa Mpango wa kitaifa wa kurasimisha makazi kwa kukopesha wananchi gharama ya kupanga, kupima na kupewa hati kwa kushirikiana na Benki ya NMB.*



# IFANYENI ARDHI KUWA MTAJI HAI
## - MARY MAKONDO



**Na. Lusajo Mwakabuku**
**WANMM, Mbeya**

Katibu Mkuu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mary Makondo amewaagiza watumishi kutoka Wizara ya Ardhi na wale wanaotoka Chuo Kikuu Ardhi kutekeleza majukumu yao katika kuhakikisha wanaifanya urasimishaji sehemu kubwa ya Tanzania ambayo haujatambuliwa kisheria ili kuipa uhai utaoleta tija ya kiuchumi kwa mahitaji ya kila siku ya watanzania.

Katibu mkuu huyo ameyasema hayo alipokuwa anatoa salamu za utangulizi katika kikao kilichojumuisha wawakilishi kutoka benki ya NMB, Chuo Kikuu Ardhi, Manispaa na Halmashauri za Mkoa wa Mbeya na viongozi na watumishi wengine kutoka Wizarani walipokutana wilayani Mbarali katika kikao cha pamoja kabla ya kuzindua rasmi mpango wa kitaifa wa urasimishaji makazi.

Akibainisha malengo makuu ambayo serikali imekusudia kuyafanya katika sekta ya Ardhi, Katibu Mkuu alisema lengo kuu ni kuhakikisha kila kipande cha Ardhi nchini kinapimwa ili kumwezesha mmiliki kuwa na haki mbalimbali zinazoambatana umiliki wa ardhi moja wapo ikiwa ni kumuinua mwananchi kiuchumi.

"Unaweza kumiliki eneo kubwa sana na likawa na mali nyingi lakini kama eneo lako hulimiliki kisheria maana yake lipo hatarini kuingia kwenye migogoro au kupangiwa matumizi mengine bila mmiliki kuwa na haki ya fidia, ni wajibu wetu kuhakikisha kwa wale wananchi wanaokuwa tayari kumilikishwa maeneo yao basi sisi wataalamu tuhakikishe tunawajibika kwa mujibu wa sheria kuzilinda milki zao ili wamiliki ardhi iliyo hai kisheria" Alisema Katibu Mkuu.

Aidha Katibu Mkuu ameishukuru benki ya NMB kwa kukubali kuunganisha nguvu na Wizara pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha kuwa mwananchi wa hali ya chini naye anamiliki ardhi yake kihalali na kuwa na maamuzi yake katika kujikwamua kiuchumi.

# ARU YAJIPANGA KUDHIBITI MAKAZI HOLELA KATIKA MIJI INAYOIBUKIA



## Na. Lusajo Mwakabuku WANMM, Mbeya

Chuo Kikuu Ardhi (ARU) kwa kushirikiana na serikali kimedhamiria kuboresha na kudhibiti makazi holela katika miji inayoibukia unaosababishwa na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa kanzi data, ramani za msingi na gharama kubwa ya kuzitengeneza kwenye Halmashauri zetu huku ikiboresha modeli ya urasimishaji iliyopo kwa lengo la kuleta matokeo chanya zaidi kwa wakazi na hivyo kuzuia makazi holela yasiendelee.

Akimwelezea mgeni rasmi katika uzinduzi wa mpango maalum wa kurasimisha makazi, Dkt. Victoria Mwakalinga ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu Ardhi na msimamizi wa mradi wa urasimishaji ardhi unaotekelezwa na Chuo Kikuu Ardhi wilayani Mbarali alisema waliamua kujikita katika urasimishaji baada utafiti uliofanywa kutambua mahitaji ya jamii katika wilaya hii.

“Baada ya kufanya utafiti wa kubaini hali halisi ya mahitaji wilayani hapa tukaona kuna umuhimu wa kuboresha modeli ya urasimishaji iliyopo ili kuleta matokeo chanya zaidi kwa wakazi na hivyo kuzuia makazi holela yasiendelee wakati tukibaini njia sahihi ya udhibiti wa makazi yaliyorasimishwa” Alisema Dkt. Mwakalinga

Hali ya upimaji ilivyo hivi sasa, Dkt Mwakalinga amesema jumla ya viwanja 5,000 (sawa na asilimia 9.6) vimekwisha pimwa, na ramani zake zilikwishaidhinishwa, idadi hiyo ndogo inatoka na idadi ndogo ya watu waliokamilisha michango yako kwani upimaji huu umefanywa kwa watu waliokamilisha michango yao tu.

“Hatua hii ya serikali kufanya mazungumzo na benki ya NMB na kufikia muafaka wa kuwawezesha wananchi kuweza kumudu gharama hizi ni ya manufaa makubwa kwetu kwani sasa tutakuwa nauhakika wakufanya kazi yetu na kuimaliza kwa wakati”
Aliongeza Dkt. Mwakalinga.




*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi (kushoto) akimtambulisha Dkt. Victoria Mwakalinga ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu Ardhi na msimamizi wa mradi wa urasimishaji ardhi unaotekelezwa na Chuo Kikuu Ardhi wilayani Mbarali*



*Baadhi ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu Ardhi wanaofanya kazi za urasimishaji wakiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Ardhi pamoja na Msimamizi wao Dkt. Victoria Mwakalinga*

# WAKUU WA WILAYA NA MIKOA WAAGIZWA KUANZISHA MADAFTARI YA MIGOGORO YA ARDHI

**Na. Hassan Mabuye,**
MBEYA

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi amezitaka ofisi zote za Wilaya na Mikoa kuwa na Daftari maalumu la orodha ya migogoro ya ardhi ili kuitambua na kuitatafutia ufumbuzi wake kwa wakati.

Waziri Lukuvi ameyasema hayo alipokutana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Mbarali mkoa wa Mbeya alipokuja kuzindua Mpango wa maalumu wa kukopesha wananchi gharama ya kupanga, kupima na kupewa hati kwa kushirikiana na Benki ya NMB.

Lukuvi amesema katika maeneo mengi nchini kumekuwa na migogoro inayoibuka kila mara na haipatiwi ufumbuzi wa kudumu na mengine imekuwa ikiibuka kwa kushtukiza kwa kuwa inatatuliwa bila kushirikisha wataalamu wa ardhi na haijawekewa mipango ya kuitatua.

"Tunajua ipo migogoro ya ardhi inayosababishwa na mipaka ambayo imeanzishwa na mamlaka, ipo migogoro ya mipaka ya kijiji na kijiji, wilaya na wilaya, hifadhi na wananchi na mipaka ya utawala. Basi tuijue migogoro hii ili tupate kuitafutia ufumbuzi na kuitatua" amesema Lukuvi.

Katika hatua nyingine Waziri Lukuvi amezitaka halmashauri za wilaya kusimamia sheria katika usimamizi wa ardhi kwa kuwa kwa Tanzania mamlaka za upangaji wa ardhi yetu ni halmashauri za wilaya sababu ndio wenye ardhi iwe ya mjini au ya vijijini.

Ameongeza kwa kusema kuwa, uvunjaji wa sheria za ardhi umekuwa ni mkubwa sana kwa maana watu wamekuwa wakijenga hovy hovyo bila vibali vya ujenzi. Maeneo mengi watu wamejenga mpaka kwenye vyanzo vya maji, wanajenga katika viwanja ambavyo havikupimwa tena nyingine ni nyumba kubwa zinajengwa bila hata kupewa onyo.

"Ninatoa maelekezo kwa wakurugenzi wote nchi nzima watowe barua kwa watendaji wa mitaa na vijiji kwamba moja ya majukumu yao ni kusimamia uendeshaji na usimazi wa ardhi kwenye mitaa na vijiji vyao" amesema Lukuvi.

Amesema kuwa, maelekezo haya yatawawezesha kuzuia ujenzi holela, manyanyaso katika ardhi, uporaji na kusimamia ujenzi unaozingatia sheria. Jambo hili litawasaidia kupata watoa taarifa za ardhi (land Rengers) na kuweza kudhibiti uonevu na uvunjifu wa sheria za ardhi.

Aidha, waziri lukuvi amezionya halmashauri ambazo husababisha kero nyingi za fidia kwa kunyanganya ardhi za watu bila kulipa fidia na kuanza kuweka miradi ya kupima viwanja na kuviuza ili kupata fedha kwa kuwa sasaivi wakurugenzi wengi wameishajua kwamba ardhi ni mali. Amezitaka halmashauri zote kuondoa kero hii ya fidia kwa kutenda haki ya kuwalipa wananchi fidia stahiki na kwa wakati bila kuzalisha migogoro mipya ya ardhi.





*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Lukuvi akiendesha kikao cha ndani na kutoa maagizo kabla ya kwenda kuzindua mpango wa kitaifa wz kurasimisha Makazi*

# MATUKIO KATIKA PICHA




















